**HOTUBA YA MHE. HAMZA SAIDI JOHARI, MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI, KATIKA MAADHIMISHO YA SIKU YA SHERIA NCHINI - VIWANJA VYA MAHAKAMA YA TANZANIA, TAMBUKARELI - DODOMA TAREHE 02 FEBRUARI, 2026**

**Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;**

**Mhe. George Mcheche Masaju, Jaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania;**

**Mhe. Mussa Azzan Zungu, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;**

**Mhe. Dkt. Juma Zuberi Homera, Waziri wa Katiba na Sheria;**

**Mhe. Khamis Ramadhan Abdallah, Jaji Mkuu wa Zanzibar;**

**Wahe. Majaji wa Mahakama ya Rufani na Mahakama Kuu ya Tanzania;**

**Mhe. Dkt. Mustapher Mohamed Siyani, Jaji Kiongozi;**

**Wahe. Mawaziri na Naibu Mawaziri mliopo;**

**Wahe. Majaji Wakuu Wastaafu;**

**Wahe. Majaji Wastaafu;**

**Mhe. Msajili Mkuu na Mtendaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania;**

**Mkurugenzi wa Mashtaka;**

**Wakili Mkuu wa Serikali;**

**Mwandishi Mkuu wa Sheria;**

**Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama;**

**Rais wa Chama cha Wanasheria wa Tanganyika;**

**Wahe. Mabalozi na Wawakilishi wa Mashirika ya Kimataifa;**

**Viongozi wote wa Taasisi za Kiserikali na Zisizo za Kiserikali mliopo;**

**Ndugu zangu Mawakili;**

**Viongozi wa dini;**

**Viongozi wa vyama vya siasa;**

**Wageni wote waalikwa;**

**Mabibi na Mabwana.**

**KAZI NA UTU .....**

**Mheshimiwa Rais,**

Awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukutana mahali hapa leo tukiwa salama. Aidha, nichukue fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Mhe. Rais, kwa uongozi imara, thabiti, makini na wenye maono unaoendelea kuimarisha mfumo wa utoaji haki nchini kwa kuzingatia misingi ya kidemokrasia, utawala bora na utawala wa sheria.

Vilevile, napenda kumpongeza Mhe. Jaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania kwa uongozi wake mahiri na wenye dira unaoendelea kuimarisha utendaji kazi, ufanisi na uhuru wa Mahakama. Namshukuru pia kwa kuialika Ofisi yangu kushiriki katika maadhimisho haya muhimu ya kitaifa.

Leo ni siku muhimu na fursa ya kufanya tafakuri ya kitaifa tunapoadhimisha Siku ya Sheria Nchini. Siku hii ni kioo kinachotukumbusha dhima na wajibu wetu wa pamoja katika kulinda amani, haki, usawa na utawala wa sheria kama nguzo na nyenzo katika kufikia ustawi na maendeleo ya Taifa.

**Mheshimiwa Rais,**

Siku ya leo inaashiria mwanzo rasmi wa mwaka mpya wa utekelezaji wa majukumu ya kikatiba ya Mahakama ya Tanzania kama Mhimili muhimu wa Dola katika utoaji wa haki. Ni jambo la kutia moyo kuona kuwa mapendekezo mengi ya Tume ya Haki Jinai uliyoiteua mwaka 2023 yameanza kutekelezwa, na yale machache yaliyosalia, ikiwemo kutungwa kwa Sheria ya Dhamana, yako katika hatua za mwisho za utekelezaji.

**Mheshimiwa Rais,**

Napenda kukupa pongezi za dhati kwa hatua madhubuti unazoendelea kuchukua katika kushughulikia changamoto zilizojitokeza baada ya Uchaguzi Mkuu, Oktoba 29 mwaka 2025, hususan kwa kuunda Tume ya Uchunguzi ambayo itaweka msingi wa Maridhiano ya Kitaifa. Hatua hizi ni

msingi muhimu katika kujenga na kudumisha umoja na mshikamano wa kitaifa, kurejesha imani ya wananchi kwa taasisi za dola na kuimarisha mazingira ya haki, amani na utulivu nchini.

**Mheshimiwa Rais,**

Tunapoadhimisha Siku ya Sheria Nchini, kila mwaka huwa na kauli mbiu yake mahsusi. Kwa mwaka huu maadhimisho haya yanafanyika chini ya kauli mbiu isemayo: "**Mchango wa Mahakama katika Ustawi na Maendeleo ya Taifa**." Kauli mbiu hii inaakisi nafasi ya kipekee ya Mahakama katika kulinda haki, kudumisha amani na kuweka mazingira wezeshi ya kisheria, kimuundo na kitaasisi kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Aliyewahi kuwa Jaji wa India, Justice S. M. Daud aliwahi kusema, nikimnukuu;

*"The judiciary is the backbone of a nation, without it, development is a myth."* Kwa tafsiri isiyo rasmi akimaanisha, Mahakama ni uti wa mgongo wa Taifa, bila yenyewe, maendeleo ni hadithi za kubuni.

**Mheshimiwa Rais,**

Naomba niseme kuwa, kwangu mimi kama Mwanasheria Mkuu wa Serikali, nimefurahishwa sana na uchaguzi wa kauli mbiu ya mwaka huu. Kauli mbiu hii inaletwa katika kipindi ambacho dunia yote ipo katika vita vya uchumi wa kijiografia na ule wa kisiasa, kwa kiingereza "geo economics na geo politics". Kwa sasa kila nchi inachukua hatua za makusudi kutumia kama si nguvu ya kisiasa au kiuchumi, basi rasilimali za asili, eneo, hali ya hewa, na uhusiano na nchi nyingine katika kukuza na kuendeleza uchumi na kuleta maendeleo kwa Taifa lake.

**Mheshimiwa Rais,**

Tumeshuhudia katika awamu yako, ukiifungua Nchi kwa kasi na sote ni mashahidi wa Miradi mikubwa iliyoanzishwa na iliyo katika hatua za majadiliano, katika sekta mbalimbali ikiwemo uchukuzi, ujenzi, nishati, madini, huduma za jamii na kadhalika. Hii ni ishara kuwa, Serikali yetu kwa kushirikiana na Mhimili wa Mahakama na Bunge imeweka mazingira rafiki ya kuvutia uwekezaji na hivyo kukuza uchumi na maendeleo ya Nchi, kupitia uingizaji wa mitaji na teknolojia na upatikanaji wa ajira.

**Mheshimiwa Rais,**

Iko fikra kwa baadhi ya watu kuwa, ustawi na maendeleo ya Taifa huletwa na Serikali pekee. Fikra hii si sahihi, kwani katika jamii na Taifa lolote, ustawi wake na maendeleo ni matokeo ya Mihimili yote mitatu; Serikali, Bunge na Mahakama, vikifanya kazi kwa kutegemeana. Wakati Serikali huchangia ustawi na maendeleo ya Taifa, kupitia majukumu yake ya kiutendaji na kibajeti, Bunge hufanya hivyo kupitia wajibu wake wa kiuwakilishi na utungaji wa sheria. Mahakama ina jukumu la kikatiba la kutafsiri na kutumia sheria na hivyo kuweka mazingira wezeshi ya kisheria kwa utekelezaji bora wa sera, mipango na miradi inayotegemewa katika kuleta ustawi na maendeleo katika Taifa.

**Mheshimiwa Rais,**

Ni bayana kuwa, Mahakama kama mlezi wa Katiba, mlinzi wa haki za binadamu na utawala wa sheria, ni nguzo muhimu katika kukuza na kuendeleza ustawi na maendeleo ya Taifa. Mahakama iliyo huru na yenye kuheshimika na kuaminika huhakikisha utekelezaji thabiti wa mikataba, ulindaji wa haki za mali na kudhibiti matendo ya matumizi mabaya ya

madaraka, ambayo hatimaye hukuza imani ya wawekezaji na hivyo kuwezesha ukuaji imara na endelevu wa uchumi wa Taifa.

Aliyewahi kuwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa; Ban Ki-moon aliwahi kusema haya, namnukuu;

*“An independent judiciary is a country’s best guarantee of fairness, justice, and development”*. Kwa tafsiri isiyo rasmi akimaanisha kuwa; Mahakama huru inahakikisha usawa, haki na maendeleo ya nchi.

**Mheshimiwa Rais,**

Naomba nieleze mambo machache yanayoonesha namna Mahakama inavyotoa mchango katika ustawi na maendeleo ya Taifa;

i. Mahakama ni kichocheo cha ukuaji wa uchumi na uwekezaji. Hili hutokea kwa kutekeleza yafuatayo;

  a. Utekelezaji wa kisheria wa mikataba; uwepo wa Mahakama inayoaminika kunahakikisha mikataba inatekelezeka na kupunguza hatari kwa wafanyabiashara, kuvutia uwekezaji wa ndani na nje na hivyo kukuza uchumi.

  b. Ulinzi wa haki za mali; Mahakama hutoa imani kwa wadau mbalimbali, mathalani wawekezaji wa muda mrefu na hivyo kuchangia katika ukuaji wa biashara na uchumi.

  c. Utatuzi wa migogoro wenye ufanisi; uwepo wa mifumo ya utatuzi wa migogoro yenye ufanisi kunawezesha mashauri mbalimbali kumalizika kwa wakati kupitia Mahakama mahsusi na hivyo kuruhusu biashara na wananchi kufanya kazi kwa ufanisi.

ii. Kuhakikisha kunakuwa na utawala wa sheria na utulivu.

   a. Mgawanyo wa madaraka; Mahakama inafanya kazi ya kuangalia utendaji kazi wa Mhimili wa Serikali na Bunge na hivyo inazuia matumizi mabaya ya madaraka kwa kuhakikisha Serikali inafanya kazi kwa mujibu wa sheria.

   b. Amani ya kijamii; kwa kuwa ni jukwa la haki na lisilo na upendeleo la kumaliza migogoro, Mahakama inalinda amani katika jamii na kuzuia uwezekano wa wananchi kuangukia kwenye kutafuta haki kupitia njia nyingine zisizo ama rasmi au zinazokinzana na sheria.

   c. Ulinzi wa haki; Mahakama inalinda Haki za msingi za Binadamu na hivyo kusaidia katika uwepo wa jamii imara, yenye usawa na jumuishi.

iii. Kukuza uwajibikaji na kuzuia rushwa.

   a. Kuzuia rushwa;  Mahakama huru inawafanya watumishi wa umma na binafsi wawajibike na hii hupunguza rushwa ambayo inaweza kuzorotesha maendeleo na kuharibu imani ya wananchi.

   b. Uwazi; mapitio ya kimahakama yanahakikisha sera na matendo ya Serikali yanafanywa kwa kuzingatia dhana ya uwazi na kufuata misingi ya kisheria.

iv. Kuwezesha maendeleo ya binadamu na jamii.

   a. Ufikiaji wa haki; Mahakama inapaswa kuhakikisha kuwa watu wote wanaifikia na kuipata haki, ikiwemo makundi

yaliyotengwa, kupunguza ubaguzi, na hivyo kuchochea ukuaji uchumi jumuishi.

b. Utekelezaji wa misingi; Mahakama ina nafasi muhimu katika kutekeleza misingi ya kimataifa ya Haki za Binadamu na misingi ya Kimataifa ya kibiashara hivyo kukuza malengo endelevu ya maendeleo.

**Mheshimiwa Rais,**

Ili Mahakama iweze kutoa mchango muhimu katika ustawi na maendeleo ya Taifa, ni lazima iwe na sifa zifuatazo;

i. Huru; Mahakimu na Majaji ni lazima wawe huru kutoka kwenye ushawishi, msukumo au vitisho kutoka Mhimili mwingine, vyama vya siasa au nguvu zozote za nje.

ii. Weledi; Mfumo mzuri wa Mahakama ni lazima upunguze msongamano wa mashauri (case backlogs) na uhakikishe unatoa haki kwa wakati.

iii. Uadilifu; Mahakimu na Majaji ni lazima wawe ni watumishi wenye uadilifu wa hali ya juu sana, na wahakikishe kunakuwa na imani ya umma katika mfumo wa sheria.

**Mheshimiwa Rais,**

Mpaka sasa, Nchi yetu imeshuhudia mabadiliko makubwa katika mfumo mzima wa utoaji haki. Haya yote yametokea kutokana na utayari wa Serikali kuhakikisha Mahakama inatoa mchango muhimu katika ustawi na maendeleo ya Taifa. Ningependa nirudie tena kukupongeza wewe Mheshimiwa Rais, kwani katika uongozi wako, Nchi yetu imeshuhudia

mabadiliko chanya na makubwa kwa upande wa Mahakama. Tunajivunia mabadiliko na maboresho mbalimbali ikiwemo;

i. Ongezeko la Majaji, Mahakimu na Mawakili;

ii. Kupungua kwa msongamano wa mashauri Mahakamani na katika Mabaraza mbalimbali;

iii. Matumizi ya mifumo ya kisasa katika kupokea, kuhifadhi na kutoa taarifa;

iv. Uboreshaji wa mazingira ya kazi, ikiwemo vitendea kazi, na ukarabati na ujenzi wa majengo ya Mahakama katika ngazi zote;

v. Kuongezeka kwa imani ya wananchi kwa mfumo wa kisheria;

vi. Kuongezeka kwa mafunzo ya Majaji, Mahakimu na Mawakili;

vii. Kuimarika na kuongezeka kwa matumizi ya TEHAMA, ikiwa ni pamoja na uwasilishaji wa nyaraka mbalimbali (E-filing) na uendeshaji wa mashauri kwa njia ya mtandao;

viii. Kuanzishwa kwa taasisi mbalimbali zenye dhima ya kuboresha sekta na mfumo wa sheria, ikiwa ni pamoja na Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria.

**Mheshimiwa Rais,**

Mahakama haifanyi kazi peke yake, bali wakati wote hushirikiana na wadau wengine katika kufikia lengo lake kuu la utoaji wa haki. Miongoni mwa wadau wakubwa wa Mahakama ni Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na taasisi zilizo chini yake, ambazo ni Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na

Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria zimeendelea kutekeleza majukumu yake katika kuhakikisha kuwa wananchi na wadau wote wanaifikia haki kwa wakati na hivyo kuchochea ustawi wa mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla. Kwa ufupi niyataje machache yanayotekelezwa na yanayoendelea kutekelezwa na Ofisi zetu hizi:

i. Upekuzi wa mikataba ambao umesaidia kuhakikisha mikataba inatekelezeka na inazingatia misingi yote ya sheria; Katika mwaka wa fedha 2024/2025, jumla ya mikataba 3,436 na hati za makubaliano 729 zilifanyiwa upekuzi na Ofisi yangu;

ii. Mageuzi ya kimuundo katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambayo yameleta ufanisi na tija kubwa katika mnyororo mzima wa utoaji na usimamizi wa haki;

iii. Uanzishaji wa Kamati za Ushauri wa Kisheria na Kliniki za sheria katika mikoa na wilaya mbalimbali Nchini. Kliniki hizo, zimetoa huduma za kisheria kwa wananchi wengi na hivyo kupunguza wingi wa mashauri na kuokoa gharama za kifedha na muda wa Mahakama na wananchi ambazo zingetumika iwapo mashauri husika yangeendeshwa Mahakamani. Hadi sasa Kamati hizi zimezinduliwa katika mikoa mitano ya Dodoma, Kilimanjaro, Manyara, Singida na Mwanza. Tangu kuanzishwa kwake mwaka 2024, Kamati zimehudumia zaidi ya wananchi 2,252 kupitia Kliniki za Sheria ambazo zinaendeshwa na Mawakili wa Serikali, Mawakili wa Kujitegemea na watoa huduma za kisheria wengine. Katika kutekeleza jukumu hili, Ofisi yangu itaendelea kushirikiana kwa karibu na wadau wote, ikiwemo Wizara ya Katiba na Sheria, Chama cha Mawakili wa Kujitegemea Tanzania (TLS), Chama cha

Mawakili wa Serikali (TPBA), Wakuu wa Mikoa na Wilaya katika kushughulikia na kutatua malalamiko ya wananchi yenye mwelekeo wa kisheria kwa wakati na kwa haki.

iv. Urekebu; Ofisi yangu imefanya maboresho na ufasili wa sheria mbalimbali ambao umesaidia kupata rejea za sheria kirahisi. Katika mwaka wa fedha 2024/2025, miswada 16 ya sheria iliandaliwa, sheria ndogo 1,018 ziliandaliwa na sheria 446 zilifanyiwa urekebu. Kwa sasa, tuko katika hatua za mwisho za kukamilisha toleo la ufasili wa sheria, na zaidi ya sheria 446 zimetafsiriwa kwa lugha ya kiswahili. Baada ya kukamilika, toleo hili litatolewa bure kwa wananchi, ikiwa ni utekelezaji wa maelekezo yako katika kuhakikisha wananchi wanazifahamu na kuzifikia haki zao.

Mfano mzuri ni mabadiliko ya sheria mbalimbali Na. 8 ya mwaka 2018 ambayo yamerekebisha Sheria ya Mahakama ya Rufaa, Sura 141 kwa kuweka kanuni iitwayo “overriding objective” au “oxygen principle”. Kanuni hii inasisitiza Mahakama kutenda haki pasipo kufungwa na mambo ya kiufundi (technicalities) pasipo sababu za msingi ili kuendana na malengo ya Ibara ya 107A (2) (e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa sasa, Ofisi yangu kwa kushirikiana na Mahakama, na wadau wengine, tuko katika hatua za mwisho za uandaaji wa Muswada utakaoimarisha vyombo vya kinidhamu kwa Maafisa Mahakama na Muswada wa kuyaingiza Mabaraza ya Ardhi na Nyumba katika mfumo rasmi wa Mahakama.

v. Katika kukabiliana na kasi ya mabadiliko ya teknolojia na mahitaji ya sasa ya utoaji huduma, Ofisi yangu imejielekeza katika matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano. Katika kufanya hivyo, tumeanzisha mifumo rahisi kama OAG-MIS ambayo imeunganishwa na mifumo ya taasisi nyingine za utoaji haki. Mifumo hiyo, imekuwa msaada mkubwa kwa wananchi katika kupata huduma na kuzifikia kwa urahisi sheria mbalimbali. Hatua hii pia imehusisha uboreshaji wa huduma za maktaba za kisheria, usimamizi na upekuzi wa mikataba pamoja na utoaji wa ushauri wa kisheria kwa njia za kidijitali, kwa lengo la kuongeza uwazi, ufanisi na uwajibikaji na tija.

vi. Ongezeko kubwa la Mawakili wa Serikali katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria.

vii. Ujenzi wa majengo ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka katika mikoa mbalimbali Nchini, na ufunguaji wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka katika jumla ya mikoa yote na wilaya 118 nchini.

viii. Kuwezesha majadiliano na usuluhishi wa mashauri nje ya Mahakama;

ix. Ofisi yangu inaendelea kuwekeza katika ujenzi wa Maktaba Mtandao, uanzishaji wa Kituo cha Huduma kwa Wateja, pamoja na mifumo ya kisasa ya usimamizi wa mikataba kwa njia ya mtandao. Aidha, mafunzo ya ndani na nje ya nchi yanaendelea kutolewa kwa Mawakili wa Serikali ambao pia ni Maafisa wa Mahakama, ili

kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa weledi na ubora unaoendana na matakwa ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.

x. Kwa kushirikiana na Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania na wadau wengine, tunaendelea kufanya tafiti na mapitio ya kisheria yanayolenga kuboresha mifumo ya utatuzi wa migogoro nje ya Mahakama. Hatua hizi zinalenga kupunguza msongamano wa mashauri mahakamani, kuongeza ufanisi wa utoaji haki na kuweka mazingira bora ya uwekezaji na hivyo kuongeza kasi ya maendeleo ya kiuchumi.

**Mheshimiwa Rais,**

Maboresho haya na jitihada zote zinazofanywa na Ofisi yangu, zinanuia kufikisha huduma za sheria kwa wananchi na wadau wote wa maendeleo bila kujali ubaguzi, na hivyo kuisadia Mahakama katika kutekeleza jukumu lake la msingi la kutoa haki.

**Mheshimiwa Rais,**

Mnamo tarehe 17 Julai, 2025 ulizindua rasmi Dira ya Taifa ya Maendeleo ya miaka 25, maarufu kama “Dira 2050”. Katika hotuba ya uzinduzi, ulibainisha kuwa, dira ni mpango jumuishi, uliobeba maono ya masafa marefu, yakiakisi matarajio na matamanio ya Watanzania kwa kipindi cha miaka 25 ijayo. Aidha, uliueleza Umma wa watanzania kuwa, ili kufikia dira ya kuwa Nchi ya Uchumi wa Kati Ngazi ya Juu unaoongozwa na maarifa na uchumi wa viwanda, ni lazima kila mmoja wetu ajenge na kudumisha utamaduni wa uwajibikaji unaozingatia weledi, ubunifu katika utekelezaji wa majukumu mbalimbali.

**Mheshimiwa Rais,**

Malengo na maudhui ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 yanaendana kwa karibu na utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030, Dira ya Jumuiya ya Afrika Mashariki 2050, Dira ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika 2050 pamoja na Ajenda 2063 ya Umoja wa Afrika. Nyaraka hizi zote, kwa pamoja, zinatambua umuhimu wa utawala wa sheria, haki jinai, amani, usalama na utawala bora kama nguzo za ustawi na maendeleo katika ngazi zote.

**Mheshimiwa Rais,**

Mara tu baada ya uzinduzi wa Dira, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na taasisi zilizo chini yake tulianza kuweka mikakati madhubuti ili kuhakikisha kuwa maeneo yote ya kisheria hayawi kikwazo bali yanakuwa rafiki katika kufikia malengo na matarajio ya Dira 2050. Kwa kushirikiana na wadau wengine, tayari tumeanza maboresho ya sheria, sera, mipango, malengo na mikakati mbalimbali ikiwa ni pamoja na kufanya tafiti za kitaalamu ili kuhakikisha kuwa masuala yote yahusuyo tasnia ya sheria yanafungamanishwa na malengo na shabaha ya Dira ya 2050.

**Mheshimiwa Rais,**

Mwisho, napenda kusisitiza kuwa mafanikio ya ustawi na maendeleo ya Taifa letu yanategemea kwa kiasi kikubwa uwepo wa mfumo imara wa utoaji haki ulio fanisi, unaoaminika, wenye kufikika na unaozingatia muda. Ni imani yetu kuwa, Mahakama ya Tanzania pekee haiwezi kutimiza lengo hilo. Kwa kushirikiana na wadau wote wa haki, itaendelea kubaki kuwa nguzo muhimu katika **ustawi wa taifa** na nyenzo muhimu katika kufikia **maendeleo endelevu** na **jumuishi**.

Kwetu sisi, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, daima tutaendelea kushirikiana na Mahakama katika kuhakikisha si tu tunaisaidia Mahakama kufikia maamuzi, lakini pia kuwahudumia watu wote kwa weledi, ubora, uadilifu na uaminifu ili kiu ya kila anayeikimbilia haki ikatimie kwa wakati. Aidha, tutaendelea kushirikiana na wadau wengine wote wanaohusika na utoaji haki ikiwa ni pamoja na Chama cha Mawakili wa Kujitegemea Tanzania (TLS) ili huduma za kisheria tunazozitoa zimfikie kila mtu. Milango yetu iko wazi wakati wote na kwa yeyote. Matamanio yetu makubwa ni kuona Mahakama na wadau wake wote, tukiwamo sisi, hatuwi kikwazo kwa namna yoyote ile bali, tunaitumia sheria kama nyenzo muhimu kufikia Taifa lenye ustawi na maendeleo tunayoyataka.

**Mheshimiwa Rais,**

Naomba nimalizie kwa kusema kuwa, Mahakama ni mhimili muhimu katika mnyororo mzima wa utoaji haki. Ufanisi wake una mchango mkubwa katika ustawi wa jamii yetu, kuvutia uwekezaji wa ndani na nje ya nchi, kuimarisha biashara, na kulihakikishia Taifa maendeleo ya kiuchumi kupitia uimarikaji na uboreshaji wa mifumo ya haki, na kudumisha usawa na uwajibikaji katika jamii na taifa. Kwa hakika, katika utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, Mahakama ina nafasi muhimu katika kujenga uchumi shindani, jumuishi na endelevu.

Uko usemi maarufu katika sheria unaosema kuwa;

*"Justice delayed is justice denied"* ikimaanisha haki iliyocheleweshwa ni haki iliyonyimwa.

Lakini kwa muktadha wa shughuli ya leo kuna usemi unaofahamika kuwa;

*“Justice delayed is development denied”* ikimaanisha haki iliyocheleweshwa ni maendeleo yaliyonyimwa”

Kwa kuwa tunaanza mwaka mpya wa Mahakama, nichukue nafasi hii kuwatakia nyote heri ya mwaka mpya 2026.

**Asanteni sana kwa kunisikiliza.**

Mhe. Hamza Saidi Johari

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI**